

- Iwapo mimea imetunzwa ifaavyo kila fifa linaweza kutoa lita 5 za mafuta. Mimea 10 inaweza kutoa lita 2,400 za mafuta kila mwaka na mavuno kwa jumla yanaweza kufikia tani 4 hadi 5 za mafuta kwa kila eka kwa mwaka.

### Maandalizi

Maandalizi ya mafuta yanaweza kufanyiwa nyumbani au kijijini, kulingana na kiwango chake.

- Tita zilizotolewa shambani hufinywa na matunda-madogo yanatolewa na kuoshwa halafu yanachemshwa kwa muda wa saa moja.
- Matunda-changa huondwa yakiwa na joto kwa kutumia kinu (kama ni nyumbani) au mashine maalum kama ni kijijini.
- Maji yenye joto kiasi huongezwa ili kuosha mafuta na kutenga nyuzi na mbegu. Mchanganyiko huu hutwiwa mtoni hadi mafuta yanaelea juu.
- Mafuta yanayoelea hutolewa yakachungwa na kulifadhiwa au kuuzwa.

### Matumizi ya mafuta

Mafuta haya yanatumika kutayarishia mboga, marahagwe, nyama, mchuzi wa samaki, chapati, wali na kadhalika.

Yanaweza pia kutumiwa kuondoa sabuni kijijini.



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### Watayarishaji:

Rachier, G.O. Orondo, S.G.O.K

Mambiri, G., Kisuya, L. na Ochebo, R.

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkuu wa Kituo,

Kari-Embu S.L.P. 27, Embu


Simu: (068) 20116/20873; Nukulishi: 068 30064

Baruapepe: kariembu@salphaco.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 64 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Kulima na kutayarisha mafuta ya mawase



## Utangulizi

Ni mmea unaonza kukutambulika kwa sababu mafuta yake ni ya hali ya juu ukiyalinganisha na mimea ya mafuta mengineyo. Mafuta haya yana vitamini ya A na E na hutumiwa kutengeneza sabuni na mishumaa. Matawi ya mti huu hutumiwa kuezeka nyumba.

## Mahitaji ya kimazingira

- Hali ya anga iliyo chini ya mita 1,000.
- Joto la juu (nyusi 22-27).
- Mimea iliyotandaa vizuri (milimita 1,000 kwa mwaka) na bila msimu wa ukame.
- Michanga ya *loam*, *alluvial* na *peat* ambayo hutoa maji vizuri na yenye asidi kiasi 5.
- Masaa tano na nusu ya jua kila siku.

Sehemu hizi ni kama magharibi na pwani ya Kenya kunakopandwa sukari.

Aina zinazopatikana ni:

Hybrid Delix Ghana, Bamenda x Avros kwa Magharibi ya Kenya; na  
Hybrid Tanzania x Avros kwa pwani.

Aina hizi zinaweza patikana KARI Kakamega na Mtwapa.

## Utayarishaji Ardhi na ulifadhi

### Nafasi kati ya mimea

Tumia fremu ya ncha 3 ya mita saba 7.8 katikati ya mistari na mita 9 katikati ya mimea.

### Preparation of planting holes

Mashimo yawe na upana wa sentimita 45 na undani wa sentimita 45. Tenga mchanga wa juu ili baadaye uchangananywe na FYM.

### Taratibu za kupanda

- Tia mchanga uliochanganywa na mbolea ndani ya shimo na uongeze gramu 300 za DAP.
- Toa mmea kwenye kijifuko na uisimamisha mbegu katika hiyo shimo.
- Limbika mchanga polepole hadi kufunikia shimo na uache nafasi ya mviringo ya mita moja ili uzungukia mmea mchanga huu.

### Kuzuia kwekwe

- Limia miti michanga kwa mviringo.
- Kuza mimea ya legume iwe ya kufunikia mchanga au ufunike na majani kavu na maganda ya tunda.



Kulimia mzunguko

- Ongeza mbolea mchangani kabla mimea kuzaa.

## Kutoa matawri yasiyo hitajika

Katika mashamba yenye umri chini ya miaka 5, toa majani yaliyokufa. Kwa mashamba ya zaidi ya miaka 5, wacha manjani mawili chini ya tifa la matunda.



Miti iliyo tolewa majani

## Maradhi na wadudu

Maradhi ni kama kifo cha jani la katikati la mkuki (*Central spear leaf*) na kuoza kwa basal trunk. Wadudu sugu ni wanyama wadogo na ndege.

## Kuvuna

Matunda hutokea baada ya miti kukua kwa miaka 3 hadi 4. Matunda ya zamabrau ilyokolea baadaye hupindua rangi ikiwa ya machungwa yakishaiva na machache huanguka mchangani yakiwa tayari.

- Tumia Malaysian chisel (tazama picha) au upanga kwa kuchuma tita zilizokomea.
- Kata majani huku ukishikilia matunda halafu tita la tunda ndipo lianguke mchangani.